

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Simu: +255 (0) 26 2322602
Tovuti: www.maji.go.tz
Barua pepe: ps@maji.go.tz



NBC Majengo Branch,
Barabara ya Kuu,
S. L. P. 456,
40473 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

UTEUZI WA KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU WA DAWASA

Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Mhandisi Gerson Hosea Lwenge (Mb), kwa kuzingatia mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Sheria ya DAWASA ya mwaka 2001, amemteua **Mhandisi Romanus Attilio Mwang'ingo** kuwa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Majitaka Dar es Salaam (DAWASA). Uteuzi huu unianza mara moja. Kabla ya uteuzi huu, **Mhandisi Romanus Attilio Mwang'ingo** alikuwa Mkurugenzi wa Huduma za Ufundi wa DAWASA.

Uteuzi wa **Mhandisi Romanus Attilio Mwang'ingo** unafuatia uamuzi wa aliyekuwa Afisa Mtendaji Mkuu **Mhandisi Archard Mutalemwa** kusitisha ajira yake ya Mkataba.

Tunamtakia mafanikio Mhandisi Romanus Mwang'ingo katika majukumu yake mapya.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Profesa Kitila Mkumbo', with a horizontal line underneath.

Profesa Kitila Mkumbo

KATIBU MKUU

19 Julai, 2017